

# La Lettre de la CPI Novembre 2006 #10

Cour  
Pénale  
Internationale  
International  
Criminal  
Court



Tahariri p.1 | Tarihi ya Kesi dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo p.1 | Ujumbe wa Mwendesha mashtaka p.2 | Habari za msinji kuhusu kesi ya Mwendesha mashtaka dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo p.2 | Utangazaji wa video p.2 | Maswali na majibu kuhusu mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka p.3 | Chumba cha Mukusanyo wa kesi p.4 | Chumba cha kwanza cha Utangulizi p.5 | Ofisi ya Mwendesha mashtaka - Timu inayohusika na kesi ya Lubanga p.5 | Wakili wa utetezi p.6 | Hati za sasa za kisheria za hadhira zipatikanazo kwenyi Ofisi ya Msajili p.6 | Wasimamizi wa kisheria wa wateswa p.7 |

## Tahariri

Mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka mbele ya kesi ya Mwendesha mashtaka dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo utaanzishwa tarehe 9/11.

Washiriki wote kwenye mkusanyo huo watapata nafasi ya kusikilizwa: Mwendesha mashtaka, Utetezi na wateswa. Kwa mara ya kwanza katika historia ya sheria ya kimataifa ya jinai, wateswa wataweza kutetea haki zao kupitia wawakili wao wa kisheria.

Ndani ya toleo hili la gazeti 'La Lettre de la CPI', mtasoma makala yanayohusu kesi dhidi ya Lubanga ikiwemo majibu kwa maswali yanayoulizwa zaidi, na utambulisho wa washiriki kwa taratibu za Mahakama. Ninatumaini kwamba toleo la gazeti "La Lettre de la CPI" kitawawezesha kusikia vizuri maswala yanayohusu kesi hizi. Na mtaweza kuona kwamba Mahakama inazingatia sana kanuni ya uendeshaji wa kesi ya haki na ya hadhara. Ni kwaajili ya hiyo ndio washiriki tofauti kwenye kesi hiyo watapewa fursa ya kutoa maoni yao. Pia hatuwa zitachukulika ili watu ambayo mahalifu yanachunguzwa na ofisi ya Mwendesha mashtaka yaliwaathiri wapewe habari halisi kuhusu kazi zinazoendeshwa kwenyi makao makuu ya Mahakama mjini The Hague.

Bruno Cathala, Msajili

## Tarihi ya Kesi dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo

Vifwatavyo ni vipindi vitakavyo rahisisha kuelewa harakati za kisheria. **Tarehe 03/03/2004** Hali ya Jamhuri ya Kidemokrasiya ya Kongo ililetwa mbele ya Mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

**Tarehe 23/06/2004** Mwendesha mashtaka alitangaza pendekezo lake la kufungua uchunguzi dhidi ya hali katika jamhuri ya Kidemokrasiya ya Kongo. Ofisi ya Prezidenti wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ilitowa uamzi kuhusu muundo wa Chumba cha kwanza cha utangulizi kinacho chunguza hali ya Jamhuri ya Kidemokrasiya ya Kongo. Chumba hicho kinaundwa na mwamuzi Akua Kuenyehia, mwamuzi Claude Jorda (mwamuzi prezidenti) na mwamuzi Sylvia Steiner.

**Tarehe 12/01/2006** Mwendesha mashataka aliwasilisha mbele ya Chumba cha kwanza cha utangulizi ombi la utoaji wa hati ya kukamata Thomas Lubanga Dyilo.

**Tarehe 17/01/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kiliwpatiya wateswa sita haki ya kushiriki kwenye uendeshaji mashtaka kwa kipindi cha uchunguzi unaohusu hali ya Jamhuri ya Kidemokrasiya ya Kongo.

**Tarehe 17/03/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kilitangaza hadharani hati ya kukamata; bwana Thomas Lubanga Dyilo ambaye alikuwa kizuizini Jamhuri ya Kidemokrasiya ya Kongo alihamishwa kwenda kwenyi Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

**Tarehe 20/03/2006** Bwana Thomas Lubanga Dyilo alifikishwa kwa mara ya kwanza mahakamani mbele ya Chumba cha kwanza cha utangulizi kwenye mkusanyo wa kesi hadhara.

Wakili Jean Flamme, raia wa Ubelgiji aliteuliwa na Ofisi ya Msajili kuwa wakili kwa muda wa bwana Thomas Lubanga Dyilo wakati alifikishwa kwa mara ya kwanza mbele ya waamuzi.

**Tarehe 13/04/2006** Bwana Lubanga aliamua kumfanya bwana Flamme wakili wake halisi.

**Tarehe 26/07/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kiliwakubalia wateswa tatu hali ya kushiriki kwenye taratibu katika kesi ya Mwendesha mashtaka zidhi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo.

**Tarehe 28/08/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kilipokea nyaraka za mashtaka na orodha ya alama za ushuhuda dhidi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo.

**Tarehe 05/10/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kiliamua kwamba mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka utakuwa tarehe 09/11/2006.

**Tarehe 20/10/2006** Chumba cha kwanza cha utangulizi kilimpatiya mteswa mwingine hali yakushiriki kwenye kesi hiyo.



## Ujumbe wa Mwendesha mashtaka

Thomas Lubanga Dyilo, mkuu mdaiwa wa mmoja baadhi ya wanamgambo wa hatari Ituri. Anadhaniwa kushiriki kwenye utendaji wa uhalifu wa vitani yaani kuwakubali na pia kuwatia kwanguvu kwenyi jeshi watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano na kuwashirikisha kikamilifu ndani ya mapambano. Hivi sasa yuko kizui zini ndani ya kituo cha zuizi cha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

Matarajio yangu ni kwamba, zaidi ya kipelekwa mbele ya sheria kwa bwana Lubanga Dyilo, kesi hii itaisaidia ulimwengu kujali hiki kitendo kisicho kubalika kisheria na kusisimusha ushirikiano wa kukikomesha. Kila mwaka maisha na hali ya baadaye maelfu ya watoto na jamii zao vinaharibiwa na vitendo hivi. Unyanyasajji dhidi ya watoto hawa ulimwenguni kote haukutambuliwa na wanaoutenda wamebaki muda mrefu bila kuazibowi.

Ofisi yangu ina mpango wa kuendesha taratibu zinazohusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa hatuwa moja kwa moja. Kesi dhidi ya Lubanga Dyilo kesi yetu ya kwanza, na siyo ya mwisho na mtu anaweza kuhisi kwamba itafwa na kesi nydingi zingine. Ofisi yangu inatumia sera za uchunguzi na za mashtaka zenzi malengo. Hii haizuiyi uendeleshaji wa uchunguzi kuhusu maasi ambayo bwana Lubanga Dyilo anadaiwa kutenda baada ya kukamilisha mashtaka haya.

Uchunguzi wenye malengo utafupisha kesi. Ufupi wa kesi utamaanisha pia utumiaji mzuri wa nguvu na mali. Tunatarajia kwamba njia hii ya kazi utasaidia kupunguza uingi wa washahidi wanaohitajika kwa kila kesi. Zaidi ya kuleta ufanisi kwa kurahisisha kesi, njia hii ya kazi itapunguza hatari ya majilipizi dhidi ya mashahidi, wateswa na jamii zao.

Kesi ya Lubanga ina funguwa mlango moja wa kihistoria katika kupambana na hali ya kutoadhibu na uwajibikaji kwa kutenda jinai hiyo dhidi ya watoto. Kwa hakika, kesi hii itatoa mwangwi utakaoenda mbali ya chumba cha mkusanyo wa kesi.

Luis Moreno-Ocampo,  
Mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai

## Habari za msinji kuhusu kesi ya Mwendesha mashtaka dhidi ya Thomas Lubanga Dyilo

Thomas Lubanga Dyilo alizaliwa tarehe 29/12/1960 pa Jiba, katika sekta ya Utcha, mtaa wa Djugu, wilaya ya Ituri, jimbo la Mashariki, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Anadhaniwa kuwa mwanzilishi wa "Union des Patriotes Congolais (UPC)" na "Forces patriotiques pour la libération du Congo (FPLC)", na anadhaniwa pia kuwa mkuu wa zamani wa majeshi ya FPLC na mkuu wa UPC.

Hati ya kumkamata bwana Lubanga ilitolewa ikiwa na mhuri wa siri tarehe 10/02/2006. Hali hiyo ya siri iliondolewa tarehe 17/03/2006 na Chumba cha utangulizi, siku hiyo bwa Lubanga Dyilo, akiwa kizui zini mjini Kinshasa, akapelekwa Mahakama pa The Hague.

Alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza tarehe 20/03. Ratiba ya awali ya mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka ilikuwa mwanzo wa mwezi wa sita; likini mkusanyo huu ulahirishwa mara mbili. Ukawiasi wa kwanza uliamriwa katokana na ombi la Mwendesha mashtaka Luis Moreno-Ocampo ambae alifafanua ya kwamba kutoptana na kuongezeka kwa uhasama Ituri, uchaguzi usoni wa kidemokrasia wa kwanza nichini mnamo zaidi ya myaka 40, usalama wa mashahidi na wateswa usingeweza kudhaminiwa. Ukawiasi wa pili uliamuliwa kwa ajili ya kulinda haki za bwana Lubanga, kwa kuhakikisha ya kwamba alama za ushuhuda zinazohitajika zipewe Utetezi kwa muda unaofaa, ili kutayarisha mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka. Mkusanyo huo utanza tarehe 09/11.

### Mashtaka yatakayohakikishwa :

Bwana Thomas Lubanga Dyilo anashtakiwa kwa msingi wa kupatikana na hatia kibinasi (kifungu 25 (3) (a) cha Mkataba wa Roma kwa:

- (i) uhalifu wa vitani unaotokana na kuwatia kwa nguvu kwenyi jeshi watoto wenye umri wa chini ya myaka kumi na tano, jinai inayostahili adhabu kufuatana na kifungu 8 (2) (b) (xxvi) ao kifungu 8 (2) (e) (vii) cha Mkataba;
- (ii) uhalifu wa vitani wa kuandikisha jeshini watoto wenye umri wa chini ya myaka kumi na tano, jinai inayostahili adhabu kufuatana na kifungu 8 (2) (e) (b) (xxvi) ao kifungu 8 (2) (vii) cha Mkataba, na uhalifu wa vitani unaotokana na kushirikisha kikamilifu watoto wenye umri wa chini ya myaka kumi na tano kwa mapambano, jinai inayostahili adhabu kufuatana na kifungu 8 (2) (b) (xxvi) ao kifungu 8 (2) (e) (vii) cha Mkataba.

Hivi sasa, kesi inasikilizwa mbele ya Chumba cha kwanza cha utangulizi kinachoundwa na waamuzi Claude Jorda (mwamuzi prezidenti), Akua Kuonyehia na Sylvia Steiner.



Bwana Thomas Lubanga Dyilo/ICC-CPI/Hans Hordijk

**Madondoo ya hati ya kukamata iliyotolewa dhidi ya bwana Lubanga Dyilo na Chumba cha kwanza cha utangulizi tarehe 10/02/2006.**

"[...] kuna sababu elekevu za kuamini kwamba tangu mwezi wa saba 2002 hadi mwezi wa kumi na mbili 2003 wanamgambo wa FPLC walitenda kwa kuyarudia matendo ya kuandikisha jeshini la FPLC watoto wenye umri wa chini ya myaka kumi na tano ambao walipewa mazoezi kwenye kambi za FPLC hapo Bule, Centrale, Mandro, Rwampara, Bogoro, Sota na Irumu";

"[...] kuna sababu elekevu za kuamini kwamba, wakati unaohusiana, wanamgambo wa FPLC, kwa mara nyingi walishirikisha kikamilifu watoto wenye umri wa chini ya myaka kumi na tano kwenye mapambano huko Libi na Mbau mwezi wa kumi 2002, huko Largu mwanzo wa mwaka 2003, huko Lipri na Bogoro mwezi wa pili na wa tatu 2003, pa Bunia mwezi wa tano 2003 na huko Djugu na Mongwalo mwezi wa sita 2003";

### Utangazaji wa video

Mkusanyo wa kesi utatangazwa kwenye tovuti ya Mahakama ya Kimataifa :

[www.icc-cpi.int](http://www.icc-cpi.int)

Tafadhalii, jueni ya kwamba upelekaji video kwenye tovuti unacheleweshwa dakika 30.



## Maswali na majibu kuhusu mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka

### 1. Mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka unamaanisha nini?

Mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka ni mkusanyo unakaohudhuriwa na watu wote na ambamo majaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai wataamua kama kuhakikisha ao kutohakikisha mashtaka ya Mwendesha mashtaka dhidi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo na kumpeleka mahakamani. Akiwepo bwana Lubanga Dyilo na wakili wake, Mwendesha mashtaka anapashwa kutetea kila shtaka na alama za ushahidi za kutosha, ili aweze kuthibitisha sababu kamili za kuaminisha ya kwamba bwana Lubanga Dyilo alitenda jinai anayoshtakiwa. Mwendesha mashtaka anaweza kufanya hivyo akitumia maandishi ao ufupi wa maandishi kama alama za ushaidi na/ao kuita mashahidi.

### 2. Kwa nini mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka ulahirishwa mara mbili?

Cheleo la kwanza la mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka liliamuliwa na Chumba cha kwanza cha utangulizi (tarehe 24 mwezi wa tano) ili kuweza kujibu swala la muda unaotakiwa kwa kutekeleza hatua za kulinda usalama wa wateswa na mashahidi huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Cheleo la pili liliamuriwa na Chumba (tarehe 20 mwezi wa kenda) kwa ajili ya kulinda haki za bwana Lubanga Dyilo, kwa kuhakikisha ya kwamba alama za ushuhuda zinazohitajika zilipewa utetezi kwa wakati unaofaa ili uweze kutayarisha mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka.

### 3. Nini kilichofanyika tangu bwana Lubangu Dyilo alihamishwa na kupelekwa mahakamani kwa mara ya kwanza?

Tangu uhamisho na kupelekwa mahakamani mara ya kwanza kwa bwana Lubanga Dyilo mwezi wa tatu 2006, kulikuwepo kazi za mhimu za awamu ya utangulizi wa kesi. Madai mengi yalitolewa na pande zote kwenyi kesi na Chumba cha utangulizi kilifanya maamuzi ili kujibu kwa madai hayo yaloambatana sana sana na utangazaji wa alama za ushuhuda na matokeo ya utangazaji huo kwa ulinzi wa usalama wa wateswa na mashahidi. Madai yanayolenga ushirikishwaji wa wateswa yalikuwa pia sababu ya ubishi. Kutokana na kwamba kutambua haki za wateswa ni kipengele kipy mbele ya mahakama za kimataifa za jinai, jambo hili linazusha matatizo ya taratibu ambayo hayakuwepo mbele. Kuhusu swala la utangazaji wa alama za ushuhuda, kiisha majadiliano mengi mengi hati karibu 400 na zaidi ya kurasa 5.000 za habari, ziliwemo alama za ushuhuda za kuthibitisha mashtaka na zingine zinazoweza kufuta mashtaka zilitangazwa na kupekuliwa. Mwisho, madai ya Utetezi ya kuachia huru yalizusha maswali mengi ya kimahakama

yaliyohusisha Wakili wa Utetezi, Ofisi ya Mwendesha mashtaka, Wawakilishi kisheria wa wateswa na wakubwa wa serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo amba waliombwa kutoa maoni kuhusu jambo hilo.

### 4. Je, bwana Lubanga Dyilo alijichagulia Wakili wake?

Baada ya kukamatwa kwa bwana Lubanga Dyilo, bwana Jean Flamme, raia wa Ubelgiji, aliteuliwa na Msajili kuwakilisha kwa muda bwana Lubanga Dyilo wakati alifikishwa kwa mara ya kwanza mbele ya waamuzi tarehe 20 mwezi wa tatu 2006. Baada ya kuleta mahakamani kwa mara ya kwanza, Ofisi ya Msajili ilimpa bwana Lubanga Dyilo orodha kamili ya mawakili amba wanaridhisha vigezo vinavyohitajika kwa kuhudhuria mbele ya Mahakama. Lengo lilikuwa kumuwezesha kujichagulia wakili. Baada ya kuchunguza mitaala mbali mbali, bwana Lubanga Dyilo aliamua tarehe 13/04/2006 kumchukua bwana Flamme kama wakili wake.

### 5. Nani analipa wakili wa bwana Lubanga Dyilo?

Kufwatana na ombi la mshitakiwa, Msajili alikubali kwa muda ya kwamba bwana Lubanga ni maskini. Ilikuwa tarehe 31/03/2006. Kwa sasa Mahakama ndio inalipa gharama za utetezi wa bwana Lubanga . Lakini hatua hiyo ilichukuliwa katika kongojea Mahakama yapate hakikisho ya habari zinazokua ndani ya ombi la bwana Lubanga Dyilo.

### 6. Je, wakili wa bwana Lubanga anaweza kupinga mashtaka wakati wa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka?

Ndiyo, wakili wa bwana Lubanga Dyilo anaweza kukataa mashtaka.

### 7. Je, wakili wa bwana Lubanga anaweza kutoa alama za ushuhuda wakati wa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka?

Ndiyo, wakati wa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka Wakili wa bwana Lubanga anaweza kutoa alama za ushuhuda na kupinga alama za ushuhuda zinazotolewa na Mwendesha mashtaka.

### 8. Ni uamzi gani Chumba cha utangulizi kinaweza kuchukua?

Chumba cha utangulizi kinaweza:

- Kuhakikisha mashtaka ambayo kimepata alama za ushuhuda za kutosha za kuyathibitisha, na ikiwa hivyo kuendelesha kesi mahakamani. Baada ya kuhakikisha mashtaka, Ofisi ya Prezidenti wa Mahakama itaunda Chumba cha kusiliza kesi kitakacho endesha kesi hiyo.
- Kukataa kuhakikisha mashtaka ambayo hakikupata alama za ushuhuda za kutosha.

Uamzi huo hauwezi kuzuia Mwendesha mashtaka kutoa ombi lingine la kuhakikisha mashtaka kwa msingi wa alama za ushuhuda za nyongeza.

- Kuahirisha mkusanyo wa kesi na kuomba Mwendesha mashtaka kutoa alama nyingine za ushuhuda ao kufanya tena uchunguzi.
- Kuahirisha mkusanyo wa kesi na kuomba Mwendesha mashtaka kubadilisha shtaka, ikionekana kama alama za ushuhuda zinathibitisha jinai tofauti na ile mshitakiwa anakabiliwa nalo.

### 9. Wakati gani Chumba cha utangulizi kitaamua ?

Kufuatana na kanuni 53 ya Kanuni za Mahakama, Chumba cha utangulizi kitaamua na kuandika uamuzi huo siku 60 baada ya kumalizika kwa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka.

### 10. Je, Mwendesha mashtaka ana uwezo wa kubadili ao kuondoa mashtaka dhidi ya bwana Lubanga ?

Kama mashtaka inahakikishwa, Mwendesha mashtaka anaweza, baada ya kuruhusiwa na Chumba cha utangulizi na kumpasha mshitakiwa, kubadili mashtaka kabla kesi ianze. Kama Mwendesha mashtaka anahitaji kuongeza mashtaka mengine ao kubadili mashtaka na mengine mazito zaidi, mkusanyo mwinge wa kesi unapashwa kufanya ili kuhakikisha mashtaka hayo. Baada ya kuanzishwa kwa kesi, Mwendesha mashtaka, akiruhusiwa na Chumba maalum ( Trial Chamber), anaweza kuondoa mashtaka.

### 11. Itakuwa je kama mashtaka yanahakikishwa?

Mwisho wa mkusanyo wa kesi wa kuhakikisha mashtaka, kama Chumba cha utangulizi kinakubali yakwamba alama za ushuhuda zinathibitisha mashtaka, bwana Lubanga atasambishwa sasa na Chumba kingine. Kufwatana na hayo, Ofisi ya Prezidenti wa Mahakama itaunda Chumba maalum (Trial Chamber) ambacho kitaendelesha utaratibu. Chumba hicho kitawasiliana na pande zote na kitachukua hatuwa kuhusu utaratibu unaofaa ili uwe wa haki na ufanyike katika muda unaofaa. Chumba hiki kitajibu maswali mengi ikiwemo lile la lugha zitakazotumiwa kwenyi kesi.


### 12. Wapi bwana Lubanga anaweka kuzuizini ?

Tangu tarehe 17/03/2006, wakati ambapo bwana Thomas Lubanga alitolewa na kusafishwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, hadi leo, anapatikana katika kituo cha zuizi cha Mahakama ya Kimataifa ya jinai kipatikanacho ndani ya Jela ya Haaglanden pa Scheveningen mjini The Hague.



## Chumba cha Mukusanyo wa kesi

Kama vile mchoro ufwatao unaonesha, kwenyi chumba cha usikilizaji kesi kunapatikana mabao ya waamzi watatu na ya pande zote zinazoshiriki kwenyi kesi: Mwendesha mashtaka, Utetezi na Mshtakiwa, na pia Wasimamizi kisheria wa wateswa walioruhusiwa kushiriki kwa taratibu za kesi ya Mwendesha mashtaka dhidi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo.



Nafasi ya hadhira





## Chumba cha kwanza cha Utangulizi

Kufuatana na jambo kuhusu hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo iliyopelekwa kwenyi Ofisi ya Mwendesha Mashtaka; Chumba cha kwanza cha utangulizi kilipewa tarehe 05/07/2004, madaraka ya kuendesha kesi. Utungo wa Chumba uliamriwa na Prezidenti tarehe 23 juni.



**Mwamuzi Claude Jorda (Ufaransa)**  
Mwamuzi prezidenti tangu tarehe 16/09/2004



**Mwamuzi Akua Kuenyehia (Ghana)**



**Mwamuzi Sylvia Steiner (Brazili)**

## Ofisi ya Mwendesha mashtaka - Timu inayohusika na kesi ya Lubanga

Divisheni ya mashtaka ni moja wa divisheni tatu zinazounda Ofisi ya Mwendesha mashtaka (OTP). Divisheni hiyo inaundwa na wanasheria wanaohusika na kesi na pia wanaohusika na rufaa. Watakao ongoza timu inayohusika na kesi ya Lubanga ni bibi Fatou Bensouda, Mwendesha mashtaka makamu na bwana Ekkehard Withopf, mwakilishi wa kwanza wa Mwendesha mashtaka.

### Fatou Bensouda - Mwendesha mashtaka makamu



Bibi Fatou Bensouda ni raia wa Gambia. Alichaguliwa na Baraza la nchi zinazounda Mahakama kuwa Mwendesha mashtaka makamu, tarehe 08/09/2004. Anaongoza Divisheni ya mashtaka ya Ofisi ya Mwendesha mashtaka. Kabla ya kuchaguliwa, bibi Bensouda alikuwa mshauri mkuu wa kisheria

kiisha akawa mkuu wa tawi la maoni ya kisheria kwenyi Mahakama ya Kimataifa ya Watuhumiwa wa Mauaji ya Halaiki ya Rwanda (ICTR). Huko Gambia, alikuwa na vyeo mbambali ambamo kile cha Mwendesha mashtaka wa serikali na cha waziri wa sheria. Alikuwa pia mjumbe wa serikali ya Gambia kwa mikusanyo ya Komisheni za matayarisho ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

### Ekkehard Withopf - Mwakilishi wa kwanza wa Mwendesha mashtaka

Ekkehard Withopf ni wakili kutoka Ujerumani. Ni mwakilishi wa kwanza wa Mwendesha mashtaka anayeongoza timu inayohusika na kesi hii. Bwana Withopf alianza kazi Ofisini mwa Mwendesha mashtaka kwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai mwezi julai 2004.

Kabla ya hayo, bwana Withopf alikuwa wakili katika kazi zisizokuwa za serikali, profesia



msaidizi kwenyi chuo kikuu cha Wurzburg, mwamuzi kwenyi mahakama za jimbo za Wurzburg na Nuremberg, na pia kama Mwendesha mashtaka wa Korti la sheria la shirikisho la Ujerumani pa Karlsruhe. Tangu mei 1999 hadi mei 2004, bwana Withopf alikuwa mwakilishi baada ya kuwa Mwakilishi wa kwanza wa Mwendesha mashtaka kwenyi Mahakama ya Kimataifa ya Uhaliwa wa Kivita katika Yugoslavia ya zamani (ICTY).




## **Wakili wa utetezi**

Utetezi ni upande muhimu kwa kesi yoyote. Unawakilisha maslahi ya mshitakiwa mbele ya Mahakama. Mkataba wa Roma unasema kama kila mtu anadhaniwa ya kwamba hana hatia hadi wakati makosa yake yataoneshwa wazi. Kufuatana na Kanuni ya utaratibu na ushuhuda, Msajili anapashwa kukamata hatua zinazofaa ili haki za utetezi ziheshimiwe kabisa kwa ajili ya kesi ya usawa kama Mkataba wa Roma unavyoifafanua.

Kama vile inaandikwa kwenyi kanuni 21(2) ya Kanuni za utaratibu na za ushahidi, Ofisi ya Msajili ilifanya orodha ya mawakili. Tangu novemba 2006, ni watu 151 ndio walikubaliwa na wanaweza kuchaguliwa ili kufanya kazi kama mawakili mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

### **Bwana Jean Flamme - Wakili wa bwana Thomas Lubanga**



Kutokana na kupelekwa kwake mahakamani kwa mara ya kwanza, bwana Thomas Lubanga alimteua wakili Jean Flamme raia wa Ubelgiji, kuwa wakili wa utetezi.

Akiwa, tangu 1974, wakili kwenyi shirika la mawakili la Gand, bwana Flamme ni mstadi wa sheria ya jinai na sheria ya kimataifa ya jinai, wa mambo kuhusu dhima zinazotokana na weledi, wa sheria ya bima, wa sheria ya ujenzi na ya manyumba, wa sheria za biashara na sheria za urithi. Anafanya kazi pia kwenyi mahakama ya biashara ya Gand kama vile muamuzi makamu na ni mmoja wa waliounda shirika la mawakili la kimataifa kuhusu jinai.

Mwaka 2005, bwana Flamme alikuwa wakili mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Watuhumiwa wa Mauaji ya Halaiki ya Rwanda (ICTR) katika kesi ya Muvunyi. Tangu mwaka 1994 hadi mwaka 1998, wakili Flamme alikuwa mwamuzi prezidenti makamu wa shirika la *Avocats sans Frontières* Belgique na alitumikia serikali ya Ubelgiji

kama mstadi wa mpango wa uhusiano kwa sekta ya kisheria nchini Burundi.

Alikuwa Katibu mkuu wa shirika la *Avocats sans Frontières* Belgique tangu mwaka 1998 hadi mwaka 2000, na alikuwa pia mmoja wa waliounda miradi "Justice pour tous au Rwanda" na "Justice pour tous au Burundi", yenye lengo la kusaidia utetezi kwenyi kesi zipitikanazo nchini na zenye kuhusu uangamizaji na mauaji ya kinyama. Sasa ni mwenyi kuandika kitabu kuhusu uangamizaji nchini Rwanda; kitaitwa Inyenzi.

Wakili Flamme alisoma sheria kwenyi Chuo kikuu cha Gand ambako alipata digrii ya sheria na digrii kama mthibitishaji. Baada ya hayo alijifunza sheria ya Common law kwenye Chuo kikuu cha King's College cha London. Wakati huo huo, alitumika vilevile mara nyingi kama kurutu kwa makampuni za kisheria mji London.

Alizaliwa mjini Gand, Ubelgiji, tarehe 31/01/1950.

### **Bibi Véronique Pandanzyla Msaidizi wa kisheria**

Bibi Véronique Pandanzyla alipewa kazi ya kumsaidia wakili Jean Flamme katika utetezi wa bwana Thomas Lubanga Dyilo. Alikuwa mshauri wa kisheria kwa wizara ya mambo za nje ya Ubelgiji kiisha akawa memba wa Shikira la mawakili wa Ubelgiji. Ana pia uzoefu kwa mambo ya sheria ya kimataifa ya kiutu na sheria ya kimataifa ihusikayo na haki za binadamu.

Alipata digrii ya sheria kwenyi chuo kikuu *Université Libre de Bruxelles* (ULB). Anayo pia digrii ya shahada ya pilii (masters degree) ya sheria ya kimataifa ya serikali na ya watu binafsi, na kwa

mambo ya uhusiano wa mataifa na maendeleo.

### **Bwana Geoff Roberts- Afisa msaidizi anayehusika na faili za kesi**

Bwana Geoff Roberts alipewa kazi yakusaidia timu ya utetezi la bwana Thomas Lubanga Dyilo.

Bwana Roberts ni memba wa shirika la mawalikili la New-York. Anauzoeufu kwenyi sheria ya kimataifa ya jinai kwa maana alitumika kama msaidizi wa kisheria katika timu iliyotetea kesi moja mbele ya Mahakama ya kimataifa ya uhalifu wa kivita Yugoslavia ya zamani (ICTY) na pia kama mshauri mkuu kwenyi Criminal Law Policy Unit ya Home Office in London. Anayo digrii ya sheria ya kimataifa ya jinai na vita kutoka Chuo kikuu cha Nottingham. Alihitimu masomo ya ngazi ya Bachelor of Law (LL.B) hapo mwaka 2001 kwenye Chuo kikuu cha King's College London. Ni pia mwenye digrii ya sheria ya mambo ya binafsi kutoka Chuo kikuu cha Sorbonne, mjini Paris.

### **Hati za sasa za kisheria za hadhira zipatikanazo kwenyi Ofisi ya Msajili**

Ukijitaji kupata habari za sasa kuhusu hati za hivi karibuni za kisheria za hadhira zipatikanazo kwenyi Ofisi ya Msajili na zinazohusu hali na kesi zilizoletwa mbele ya Mahakama, tafadhalii uangalie kwenyi tovuti ya Mahakama :

[www.icc-cpi.int/cases.html](http://www.icc-cpi.int/cases.html)



## Wasimamizi wa kisheria wa wateswa

Moja katika mabadili yaliyoletwa na Mkataba wa Roma na Kanuni za utaratibu na ushuhuda ni haki mbalimbali zinazopewa kwa wateswa. Wakati utaratibu unaendeshwa, wateswa wana haki yakushiriki wakitoa moja kwa moja maoni na wasiwasi zao mbele ya waamuzi. Leo hii, ni watu wane ndio waliokubaliwa kuwa na hali kisheria ya wateswa na wanaruhusa ya kushiriki katika kesi ya Mwendesha mashtaka dhidi ya bwana Thomas Lubanga Dyilo. Wasimamizi wao wa kisheria ni bwana Luc Walleyn na bwana Franck Mulenda, wanawakilisha washiriki a/0001/06 hadi a/003/06, na bibi Carine Bapita Buyangandu, anayewakilisha mshiriki a/0105/06.

### Bwana Luc Walleyn - Wakili



Bwana Luc Walleyn (wa Ubelgiji) ni memba wa shirika la mawakili la Brussels tangu mwaka 1972 yeye ni pia wakili kwenye kampuni ya mawakili *Blanmailland & Partners* ya mjini Brussels. Yeye anashurulika zaidi na sheria kuhusu wageni na wakimbizi, na sheria ya kiutu, na haki za binadamu na maswali yanayohusu ubaguzi. Aliwakilisha wateswa kadhaa kwenyi kesi dhidi ya wakubwa wa serikali hasa katika kesi za "Casques bleus belges" zilizochunguza hatia zilizodhaniwa kwamba zilitendwa dhidi ya raia nchini Somalia.

Alipokuwa memba wa shirika *Avocats sans Frontières*, aliwakilisha washtakiwa kadhaa mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Watuhumiwa wa Mauaji ya Halaiki ya Rwanda (ICTR).

Bwana Walleyn alihuzuria mkusanyo wa kibalozi mjini Roma (1998) ajili ya kuundwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kama mwangalizi kutoka shirika moja lisilokuwa la serikali. Alihuzuria pia mkusanyo wa Komisheni ya Afrika ya haki za binadamu na za umma mjini Bujumbura mwaka 1999. Mwaka 2003 na 2004, alihuzuria mikusanyo ya Baraza la nchi zinazounda Mahakama ya Kimataifa ya jinai. Mwaka 2001, alihuzuria mkusanyo wa kiarabu dhidi ya ubaguzi wa

rangi. Alikwisha kushiriki kwenyi mikusanyo na semina nydingi kuhusu haki za binadamu zilizo fanyika katika maeneo mbalimbali duniani.

Wakili Walleyn ni memba mwumbaji wa shirika la mawakili Barreau pénal international na pia memba wa shirika CCPI ambamo anatumika katika kundi lihusikalo na haki za wateswa.

Alipata digrii ya sheria kwenyi chuo kikuu cha Leuven, mwaka 1971.

### Bwana Franck Mulenda - Wakili



Bwana Mulenda (Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ni wakili kwenye shirika la mawakili la Kinshasa/Gombe tangu tarehe 19/09/1986. Ni mwalimu wa mawakili kuhusu sheria ya kimataifa ya jinai na pia memba wa komisheni inayo husika na utafiti na uchapishaji kwenyi shirika la mawakili la Kinshasa/Gombe.

Alitumikia vilevile serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kama mstadi katika Ofisi ya waziri wa haki za binadamu. Alitumika pamoja na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayo husika na Haki za Binadamu (OHCHR) kama bingwa wa ukaguzi wa hesabu kwa sekta ya kimahakama ambayo iliidesha tathmini ya sheria kwa jumla.

Alitumika kwenyi Shirika la Ubelgiji Avocats

*Sans Frontières* kama mratibu wa mradi wa misaada ya kimahakama yenyi kuhusu jinai za kimataifa na hatia dhidi ya haki za binadamu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mwaka 1984 bwana Mulenda alipata digrii ya sheria ihusikayo na utaratibu wa kesi katika mambo yasiyo kuwa ya serikali (droit privé judiciaire). Ana pia degrii katika sayansi za jinai (1985) kutoka chuo kikuu Marien Ngouabi cha Brazzaville.

### Bibi Carine Bapita Buyangandu - Wakili



Bibi Bapita Buyangandu (Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) ni memba wa shirika za mawakili za Kinshasa na Kananga tangu mwaka 1995.

Yeye alikuwa prezidenti wa shirika isiyokuwa ya kiserikali (NGO) *Femmes et Enfants pour les Droits de l'Homme* (FEDHO) na mlinda fedha wa shirika la mawakili la Kinshasa/Matete. Tangu mwaka 1998 hadi mwaka 1999, alitumika kwenyi Ofisi ya Umoja wa Mataifa ihusikayo na haki za binadamu kama Human Rights Assistant nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Bibi Buyangandu alipata digrii yake ya sheria kwenyi chuo kikuu cha Kinshasa.